



BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA TATU

Kikao cha Tatu – Tarehe 01 Disemba, 2023.

**Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.**

I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Hotuba ya Uwasilishaji wa Mswada wa Sheria ya Kuweka Masharti ya Utoaji Leseni, Kudhibiti na Kusimamia Biashara ya Huduma Ndogo Ndogo za Fedha Kwa Ajili ya Kudumisha Utulivu, Usalama na Ubora wa Huduma Ndogo Ndogo za Fedha na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Bajeti Kuhusu Mswada wa Sheria ya Kuweka Masharti ya Utoaji Leseni, Kudhibiti na Kusimamia Biashara ya Huduma Ndogo Ndogo za Fedha Kwa Ajili ya Kudumisha Utulivu, Usalama na Ubora wa Huduma Ndogo Ndogo za Fedha na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

II. MASWALI:

Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

12. MHESHIMIWA ZAWADI AMOUR NASSOR (Jimbo la Konde) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Tayari Serikali imeingiza mifumo katika huduma zake mbali mbali, ikiwa ni pamoja na huduma za malipo, matibabu kwa Hospitali kubwa na huduma za kibenki. Na kwa kuwa kumekuwa na kugoma kwa mifumo hii baadhi ya wakati.

- (a) Je, kuna mbadala gani mwengine pindi mtandao ukigoma kufanya kazi hasa katika utoaji wa huduma za matibabu kwa wananchi wetu.
- (b) Je, Wizara imejipanga vipi kukabiliana na changamoto hii hasa katika sekta zinazotoa huduma za dharura mfano benki na hospitali.

Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

38. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

Ni mikutano mingapi ya kimataifa (International conferences) ambayo imefanyika Zanzibar kwa kipindi cha miaka 3 ya uongozi wa Dr. Hussein Ali Hassan Mwinyi iliyoweza kuchochea uwekezaji katika vivutio mbali mbali vya utalii na biashara.

Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

27. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Kumekuwa na baadhi ya bandari bubu tofauti katika nchi yetu ambazo kwa namna fulani zinaikosesha mapato stahiki Serikali yetu.

Je, Serikali ina mikakati yoyote ya kuziimarisha bandari bubu ili kuweza kuzuia upotevu wa mapato na usalama kwa ujumla.

Wizara ya Afya:

52. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Je, ni aina gani ya maradhi yanayoweza kuwapata watu wanaoishi karibu na maeneo yenye mlimbikano wa takataka za majaa.

53. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

- (a) Je, ni aina gani ya maradhi ambayo yakimpata mgonjwa kwa sasa ni lazima apatiwe matibabu nje ya nchi.
- (b) Ni aina gani ya misaada hupatiwa wagonjwa hawa hususan wanaoishi katika mazingira magumu.
- (c) Ni wagonjwa wangapi kwa mwaka husafirishwa kwa ajili ya kutibiwa nje ya nchi.

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:

3. MHESHIMIWA MWANTATU MBARAK KHAMIS (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha skuli zinazojengwa zinakuwa na walimu wa kutosha na vifaa vya kufundishia ili lengo la kujengwa skuli hizo lifikiwe.

43. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

- (a) Suala la wazazi kusimamia vyema mwenendo wa watoto wao mashuleni linatekelezwa vipi na Wizara yako inalisimamiaje suala hili.
- (b) Je, kwa kiasi gani suala la mwenendo mbaya wa watoto wetu mashuleni linachangia katika kupungua kwa viwango vya ufaulu katika mitihani yao.

- (c) Mbali na kuwahamasisha wazazi kusimamia mienendo ya watoto wao, je ni upi mkakati maalum wa Wizara yako katika kulisimamia suala hili.

Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

80. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

Je, tathmini iko vipi kwa mazao ya biashara hususan katika kuliingizia taifa fedha za kigeni.

III. **HOJA ZA SERIKALI:**

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Mswada wa Sheria ya Kuweka Masharti ya Utoaji Leseni, Kudhibiti na Kusimamia Biashara ya Huduma Ndogo Ndogo za Fedha Kwa Ajili ya Kudumisha Utulivu, Usalama na Ubora wa Huduma Ndogo Ndogo za Fedha na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo – Kusomwa kwa mara ya Pili.

Zanzibar,
01 Disemba, 2023.


Raya Issa Msellem
KATIBU WA BARAZA.